

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Simu Na. 2533015 au 2533016
Email:md@mbulude.go.tz
Fax Na: 027-2533016
Mbulu-Manyara
Unapojibu tafadhali taja:



Ukumbi wa Halmashauri,
S.L.P. 74,
Mbulu
Manyara

Kumb.Na.MDC/DED/S2/44/II/144

31Oktoba, 2017

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu anawatangazia Nafasi za Kazi na anakaribisha maombi ya Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza Nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

1.1 MTENDAJI WA KIJIJI III (VILLAGE EXECUTIVE III) – NAFASI 19

Nafasi hizi ni kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenyе Elimu ya Kidato cha Nne (IV) AU Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology), Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi Wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Serikali katika Kijiji
- Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika

Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;

- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua matatizo/malalamiko na migogoro ya Wananchi katika Kijiji
- Kusimamia Utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji; na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

1.1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B** kwa mwezi

NB: MASHARTI YA JUMLA.

- i. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V)
- iii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport Size) na ziandikwe majina nyuma.
- iv. **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- v. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- viii. **Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 14 Novemba, 2017 saa 9.30 Alasiri.**
- ix. Tangazo hili linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.mbuludc.go.tz
- x. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kuitia posta kwa anuani ifuatayo.

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU,
S.L.P. 74,
MBULU.**

AU

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR,
MBULU DISTRICT COUNCIL,
P.O.Box 74,
MBULU.**

**Hudson S Kamoga
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU.**